

MUHTASARI WA MRADI WA WE LIVE FOR US

We Live For Us ni mradi wa kuwafunza vijana kati ya miaka 18-25 kuhusu afya ya kiakili. Miongoni mwa mada zilizofunzwa kwenye hizi hamazisho ni kuelewa afya ya kiakili, jinsi ya kupeana huduma za dharura za afya ya kiakili na zinginezo. Zoezi hili la hamazisho kwa njia ya mafunzo teule liliwateua vijana sitini kutoka kwa jumla ya maombi 847. Haya maombi yalitumwa kupitia mitandao ya kijamii yaliyoongozwa na Shirika la Msalaba Mwekundu-Kenya na kupigwa jeki na International Mental Health Association. Hawa vijana 20 kwa kila Kaunti, waliteuliwa kutoka kwenye mashirika ya kijamii yanayolenga vijana kwenye Kaunti za mkoa wa pwani; Mombasa, Kilifi na Kwale. Hili zoezi lilifaa kuchukua siku tano lakini kwa sababau ambazo hazingeepekika, lilichukua siku tatu kwa kila kaunti.



Matokeo

Tulifanya utafiti kuelewa kiwango cha maarifa, unyanyapaa na mitazamo ya hawa vijana kuhusu afya ya kiakili. Kijumla, idadi kubwa ya waliohusika walionyesha kubadili mitazamo ya na maarifa kuhusu afya ya kiakili ikilinganishwa na data kabla ya mafunzo. Asilimia mia moja ya waliofunzwa walijitolea kuwahamazisha wenzao kuhusu mafunzo waliyoyapata. Hili kwetu ni la maana sana ukitilia mkazo unyanyapaa uliopo.



Yaliyojitokeza

1. Vijana chini Kenya wako tayari na wana nia ya kufunzwa na kuelewa afya ya kiakili. Tulikua na uwezo wa kuwafunza vijana 60 kati ya maombi 847 tuliyoapata- jambo ambalo linaonyesha pengo kubwa kati ya nia na hitaji.
2. Kuwafunza vijana ni njia kuu ya kupunguza unyanyapaa uliokita mizizi kwenye jamii zetu kote nchini.
3. Afya ya Kiakili yahitaji ushirikiano. Vijana waliopata haya mafuzo wamejotoza nyanjani kuwahazisha familia, marafiki na jamii zao kuhusu afya ya kiakili. Ni kupitia huu ushirikiano kati ya shirika letu la International Mental Health Association na shirika la Msalaba Mwekundu huu mradi uliweza kufanyika na kufanikiwa. Wale tuliowafunza sasa ni mabalozi wa afya ya kiakili wanaoeneza jumbe sahihi na kuchangia kufikia malengo ya kiafya nchini na pia ulimwenguni.

Mipango

Tuna mipango ya kuendeleza huu mradi kwenye kaunti zingine nchini siku zijazo. Ikiwa ungependa kujiunga na sisi, tutumie barua pepe kwenye teameimha.ngo. Asante.